BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

# HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA UCHUMI YA BARAZA LA WAWAKILISHI, KUHUSU MSWADA WA SHERIA YA KUFUTA SHERIA YA BODI YA MAPATO ZANZIBAR, NAM. 7 YA 1996 NA KUANZISHA MAMLAKA YA MAPATO ZANZIBAR.

**Mheshimiwa Spika,**

Awali ya yote napenda nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, mwingi wa rehema, aliyetujaalia uzima na afya njema na kutuwezesha kukutana leo hii ndani ya Baraza letu kuendelea na majukumu yetu ya Kitaifa. Namuomba Mola wetu anijaalie ufasaha katika uwasilishaji wa Hotuba hii na atupe usikivu na uelewa ili tuweze kuuchangia kwa umakini wa hali ya juu na hatimae kuupitisha mswada uliopo mbele yetu kwa maslahi ya Taifa.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa namna ya pekee napenda kuchukua fursa hii adhimu kukushukuru wewe binafsi kwa kuniruhusu kusimama mbele ya Baraza lako Tukufu ili niwasilishe maoni ya Kamati ya Uchumi ya Baraza la Wawakilishi kuhusiana na **Mswada Wa Sheria Ya Kufuta Sheria Ya Bodi Ya Mapato Zanzibar, Nam. 7 ya 1996 Na Kuanzisha Mamlaka Ya Mapato Zanzibar.**

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yangu inatoa pongeza za dhati kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa ujasiri wake katika jukumu zima la uongozi wa Nchi hii, sambamba na jitihada anazozichukua za kuendeleza sekta ya fedha na kuhuisha ukusanyaji wa mapato ya Serikali kupitia mifumo mbali mbali pamoja na kuziba mianya ya uvujaji wa mapato hayo kwa maslahi ya Taifa. Kwa kweli Mheshimiwa Rais ameamua kuongoza mapambano dhidi ya uvujaji wa mapato nasi waheshimiwa hatuna budi kumuunga mkono kwa nguvu zetu zote.

**Mheshimiwa Spika,**

Tunatoa shukurani za dhati kwa Makamo wa Kwanza wa Rais Mheshimiwa Othman Masoud Othman na Makamo wa Pili wa Rais Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla kwa namna wanavyomsaidia Mheshimiwa Rais katika jukumu zito la uongozi wa nchi yetu. Namuomba Mola mtukufu awajaaliye viongozi wetu hawa afya njema na maisha marefu ili waendelee kusimamia vyema nchi yetu na kuleta maendeleo endelevu tunayoyatarajia.

**Mheshimiwa Spika,**

Naomba sasa nichukue fursa hii kumpongeza Waziri wa nchi Afisi ya Rais Fedha na Mipango Mheshimiwa Dkt. Saada Mkuya Salum, Naibu Waziri Mheshimiwa Ali Suleiman Ameir (Mrembo) pamoja na timu ya watalaamu wa Wizara pamoja na wale wanaotoka Bodi ya Mapato Zanzibar kwa mashirikiano yao waliyoipatia Kamati yetu katika kipindi chote cha majadiliano ya Mswada huu.

**Mheshimiwa Spika,**

Napenda kuwashukuru Wanasheria wa Afisi ya Baraza la Wawakilishi pamoja na Wanasheria kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa uchambuzi na ufafanuzi wa hoja mbali mbali zilizojitokeza wakati wa kuujadili mswada huu kwenye ngazi ya Kamati. Michango yao ni muhimu katika kuujenga mswada wetu kwa maslahi mapana ya nchi yetu na watu wake.

**Mheshimiwa Spika,**

Mswada uliopo mbele yetu uliwasilishwa kwako kwa hati ya dharura. Hivyo, Kamati yetu ilipata fursa ya kuwaalikwa wadau mbalimbali ili kuujadili Mswada huo kama inavyoelekezwa na kanuni ya 84 ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi Toleo la 2020 ingawa ni kwa mwaliko wa muda mfupi mno. Aidha, Kamati yetu ilipata fursa ya kukutana na Watendaji wa Afisi ya Rais, Fedha na Mipango siku ya Jumamosi ya tarehe 26 Novemba, 2022 na kujadili juu ya mswada huu.

**Mheshimiwa Spika,**

Natoa pongezi za dhati kwa Wajumbe wa Kamati ya Uchumi kwa kazi kubwa waliyoifanya ya kuujadili na kuuchambua mswada ulioletwa mbele yao kwa upeo na ustadi wa hali ya juu. Naomba sasa niwape fursa Wajumbe wa Baraza hili kuwatambua Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati hii mmoja baada ya mwengine kama ifuatavyo:

1. Mhe. Sabiha Filfil Thani - Mwenyekiti
2. Mhe. Dkt. Soud Nahoda Hassan - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Hassan Hamad Omar - Mjumbe
4. Mhe. Panya Ali Abdalla - Mjumbe
5. Mhe. Rukia Omar Ramadhan - Mjumbe
6. Mhe. Ameir Abdalla Ameir - Mjumbe

**Mheshimiwa Spika,**

Katika uchambuzi wa Mswada huu, Kamati yangu ilifanya kazi na makatibu wetu ambao kwa kiasi kikubwa wamekuwa wakitusaidia na kuturahisishia kuuchambua ipasavyo mswada huu, naomba nao niwatambue kwa kuwataja majina yao kama ifuatavyo;

1. Ndugu Noman Thabit Noman -Katibu
2. Ndugu Asma Ali Kassim -Katibu.

**Mheshimiwa Spika,**

Mswada huu unalenga kuweka mazingira mazuri ya ukusanyaji wa mapato ya nchi kwa kuanzisha Taasisi imara zaidi ya makusanyo inayoendana na mifumo ya taasisi za ukusanyaji zenye hadhi ya Mamlaka. Hatua hii ni muhimu katika kuongeza uwajibikaji wa ulipaji kodi kwa hiari na kutoa taswira ya kuwa na Taasisi yenye mamlaka na nguvu kwa walipa kodi. Kamati yetu inaipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kuiongezea nguvu taasisi hii ambayo ndio roho ya uchumi wa Taifa letu.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yetu imefanya marekebisho kadhaa kwenye mswada huu yakiwemo marekebisho ya herufi, kuongeza aya na maneno, kufuta maneno, kuondoa makosa ya kisarufi na kuweka uwiano baina ya nakala ya mswada wa Kiingereza na Kiswahili yanayoonekana kwenye waraka wa mapendekezo ya marekebisho ambao umeingizwa kwenye vishkwambi vyetu. Kimsingi, Kamati imeridhika na maudhui, dhamira na malengo ya mswada huu.

**Mheshimiwa Spika,**

Katika kuhakikisha Mamlaka ya Mapato Zanzibar inatekeleza kazi zake kwa ufanisi, Kamati yetu imelazimika kufanya marekebisho katika kifungu cha 5

kinachozungumzia kazi za Mamlaka kwa kuongeza aya mpya ya (g) inayotoa fursa kwa Mamlaka kufanya utafiti unaohusiana na masuala ya kodi ili iweze kuanzisha kodi zitakazokuwa rafiki kwa walipa kodi na kuondosha migongano inayoweza kutokea baina ya Mamlaka na Walipa Kodi. Aidha, Mamlaka itaweza kutoa ushauri uliokuwa sahihi kwa Waziri anayehusika na kodi ili aweze kuwa na uelewa na kuiwakilisha ipasavyo Mamlaka Serikalini.

**Mheshimiwa Spika,**

Iwapo marekebisho hayo yatakosekana kuingizwa katika Mswada huu, Walipa kodi wanaweza kuhoji juu ya uhalali wa Mamlaka kwamba haina mashiko katika uanzishwaji wa kodi inazozipanga siku baada ya siku na kupelekea Mamlaka kushindwa kufikia malengo yake ya ukusanyaji nchini na kuzorotesha Mipango yetu ya maendeleo. Kwa mantiki hiyo, Kamati ya Uchumi inapendekeza kuwepo kwa aya ya (g) katika kifungu cha 5 cha Mswada huo kitakachosomeka:

"***kufanya tafiti zinazohusiana na masuala ya kodi na ukusanyaji wa mapato ili kumshaauri Waziri na taasisi nyengine husika za Serikali***."

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yetu inapendekeza kufanywa marekebisho katika kifungu cha 8 kinachoelezea Wajumbe wa Bodi ya Mamlaka kwa kumuingiza Katibu Mkuu anayehusika na masuala ya fedha au Mwakilishi wake. Kamati imependekeza marekebisho hayo ili Bodi iwe na Mwakilishi mwenye maamuzi kutoka katika Wizara inayoisimamia Mamlaka ya Mapato.

Kuwepo kwa Katibu Mkuu ndani ya Bodi hiyo, kutaleta taswira nzuri ya uwajibikaji na utawala bora nchini hasa ukizingatia yeye ndio Mtendaji Mkuu wa makusanyo na Msimamizi wa matumizi ya Serikali. Hivyo atakuwa na uwezo wa kuelekeza na kufanya maamuzi stahiki, kwa wakati stahiki na kwa jambo mahsusi litakalokuwa linafanyiwa kazi na Bodi.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yetu inapendekeza kufanyiwa marekebisho kifungu cha 8(3) ili kuwawezesha Wajumbe wanaoingia kwa nafasi zao kuwakilishwa katika vikao vya Bodi na Maafisa Waandamizi watakaotoka katika Taasisi zao iwapo watashindwa kuhudhuria vikao hivyo. Kwa mnasaba huo, Kamati yetu inapendekeza kufutwa maneno **"Mjumbe wa Bodi aliyeteuliwa na Waziri"** na kuwekwa badala yake maneno **"isipokuwa Mjumbe chini ya aya ya (e) na Wajumbe wanaoingia kwa nafasi zao".**

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa nia njema Kamati imefanya marekebisho hayo ili kuzuia uwakilishwaji katika vikao vya Bodi usifanywe kwa Wajumbe walioteuliwa na Mheshimiwa Waziri badala yake ufanywe kwa Watendaji Wakuu waliokabidhiwa dhamana mbali mbali Serikalini ili waweze kupata fursa ya kuwakilishwa na Watendaji wao Waandamizi kwa vile Wakuu hao mara nyingi huwa wanashindwa kuhudhuria vikao vya Bodi kutokana na kutingwa na majukumu mengine muhimu zaidi ya kitaifa na kupunguza ufanisi wa shughuli za Bodi kwani uwepo wao au Mwakilishi wake katika uendeshaji vikao vya Bodi ni jambo la msingi.

**Mheshimiwa Spika,**

Ili kuhakikisha Wajumbe wa Bodi wanateuliwa na Waziri kwa mujibu wa sifa na vigezo vilivyowekwa, Kamati yetu inapendekeza kuwepo kwa maelezo yaani 'proviso' itakayoelekeza uteuzi wa Wajumbe hao utawawezesha kuingia katika Vikao vya Bodi ufanywe na wao wenyewe na sio wawakilishi wao. Kufanya hivyo kutaondoa changamoto za kuwa na wajumbe wapya ndani ya Bodi kila baada ya muda pamoja na kutokuwepo kwa usiri wa maamuzi yanayofanywa na Bodi kutokana na kukosa udhibiti wa Wajumbe walioteuliwa na Waziri kama unavyoeleza Mswada hivi sasa.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa kutambua umuhimu wa kazi za Katibu wa Bodi ya Mamlaka hii, Kamati yetu ilikipitia kwa kina kifungu cha 11 kilichomuelezea Katibu wa Bodi pamoja na kazi zake na kugundua kwamba kuna kazi moja muhimu na ya msingi ambayo haijaainishwa katika kifungu hicho kuhusiana na uandaaji wa agenda za vikao vya Bodi.

**Mheshimiwa Spika,**

Katika kutathmini jukumu hilo, Kamati yetu imeenda mbali zaidi kwa kuangalia jukumu hilo litatekelezwa kwa utaratibu gani na kupendekeza kwamba uandaaji wa agenda hizo utatekelezwa kwa kushauriana na Mwenyekiti wa Bodi. Kamati imeona jukumu hili asiachiwe Katibu peke yake kwa vile Mwenyekiti wa Bodi ndiye Msimamizi Mkuu wa Bodi, hivyo ni lazima ashirikishwe katika uandaaji wa agenda zinazohusu mambo yote atakayoyasimamia.

**Mheshimiwa Spika,**

Baada ya kupitia kwa undani kifungu cha 12 kinachoelezea kazi za Bodi, Kamati yangu inapendekeza kufutwa kwa aya ya (g) ya kifungu hicho kwa

vile maana halisi ya aya hiyo haileti taswira ya kazi ambayo Bodi inatakiwa izitekeleze. Badala yake, Kamati inapendekeza kuingizwa aya nyengine inayoipa Bodi kazi ya kuchukua hatua za kinidhamu kwa watumishi wa Mamlaka wanaokwenda kinyume na Sheria, Kanuni, Maadili na Viwango vya kiutendaji vinavyohitajika na Mamlaka.

**Mheshimiwa Spika,**

Katika kuhakikisha Mswada huu wa kuanzisha Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) unaenda sambamba na vigezo vya Kitaifa, Kimataifa na Sheria zinazohusiana na uanzishaji wa Mamlaka za Mapato, Kamati yetu inapendekeza kufanyika kwa marekebisho katika kifungu cha 20 kwa kuuweka sawa muundo wa Mamlaka ya Mapato Zanzibar kwa kuwapanga vizuri viongozi wake kwa mujibu wa nafasi watakazozitumikia. Hivi sasa mswada umeonesha Wakuu wa Idara na Divisheni kwa ujumla wake badala ya kuonesha vyeo vya Watendaji hao ikijumuisha Makamishna, Wakurugenzi, Mameneja na Wakuu wa Vitengo na isomeke kama ifuatavyo:

**20(1) "Mamlaka inaweza kuanzisha idara, divisheni na vitengo itakapoona inafaa kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Utumushi wa Umma.**

**(2) Makamishna na Wakurugenzi wa idara watateuliwa na Bodi kwa kuzingatia utaratibu wa ushindani utakaowekwa na Bodi.**

**(3) Mameneja na Wakuu wa Vitengo watateuliwa na Kamishna Mkuu kwa kuzingatia sifa na uzoefu wao.**

**(4) Makamishna, Wakurugenzi, Mameneja na Wakuu wa Vitengo watawajibikwa kwa Kamishna Mkuu."**

Kufanya hivyo kutawasaidia watumiaji wa Sheria hii yaani Walipa kodi wetu kuelewa kwa urahisi muundo wa Mamlaka yao na kutambua uwajibikaji wa watendaji wanaosimamia Mamlaka hiyo.

**Mheshimiwa Spika,**

Sheria za Uanzishwaji wa Mamlaka za Mapato kama hii Ulimwenguni, zinakuwa zikielezewa kiuwazi kuhusu upatikanaji wa fedha zitakazotumika katika uendeshaji wa Taasisi hizo. Katika kulitekeleza hilo, kunakuwa na kifungu maalum ndani ya Sheria hizo kinachotoa uwezo kwa Mamlaka kuzuia asilimia fulani ya makusanyo *(retention)* inayoyofanya kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za Mamlaka, utoaji wa uelewa wa masuala ya kodi,

ufanyaji wa oparesheni tofauti pamoja na kutekeleza mambo mengine kwa maslahi na mustakabali mwema wa Mamlaka hizo.

Kuhakikisha hilo linafanyika, Kamati yetu inapendekeza kifungu cha 24(1) kirekebishwe ili kuipa Mamlaka yetu hii uwezo wa kuzuia asilimia ya fedha inayotokana na makusanyo yaliyopatikana. Hivyo, Kamati inapendekeza kifungu cha Sheria ya awali kirudishwe katika Mswada huu ili Mamlaka yetu hii iweze kuwa na miguu ya kusimama yenyewe.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati ya Uchumi inapendekeza kuongezwa kwa kifungu kipya cha 39 ambacho kitampa uwezo Mheshimiwa Waziri kutunga Kanuni zitakazohakikisha utekelezaji bora wa Sheria hii baada ya kutiwa saini na Mheshimiwa Rais na kuwa Sheria kamili.

Ingawa utekelezaji wa Sheria hii utategemea Kanuni zilizotungwa kwa mujibu wa Sheria zinazohusiana na mapato Zanzibar ambazo katika Sheria hii zimetambuliwa kama ni sehemu ya utekelezaji wake lakini kuna uwezekano mkubwa wa kutokea baadhi ya mambo yatakayohitaji kukaziwa nguvu utekelezaji wake kwa Kanuni ambayo utungaji wake hauna utaratibu mrefu kama ilivyo katika utungaji wa Sheria.

**Mheshimiwa Spika,**

Marekebisho mengine yaliyopendekezwa na Kamati ya Uchumi yameainishwa kwenye waraka wa marekebisho ambao tayari umeingizwa kwenye mfumo wa Baraza mtandao.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa kumalizia, natoa shukurani za dhati kwa Wajumbe wote wa Baraza lako Tukufu kwa utulivu na usikivu wao wakati wote wa uwasilishaji wa taarifa yetu na naomba tuuchangie, tuujadili, tutowe mapendekezo na hatimae tuupitishe mswada huu.

**Mheshimiwa Spika**,

Kwa niaba ya Kamati yangu, naomba kuwasilisha.

Ahsante,

................................
Mhe. Sabiha Filfil Thani,
Mwenyekiti,
Kamati ya Uchumi,
Baraza la Wawakilishi,
**Zanzibar.**